TANGAZO LA SERIKALI NA. 741 la tarehe 30/11/2018

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA. 287)

_____

SHERIA NDOGO

_____

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153

SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE, 2018

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze za mwaka 2018 na zitaanza

Matumizi

kutumika baada ya kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali

Tafsiri

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri yaWilaya ya Chalinze

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

" Afisa Mwidhiniwa ''maana yake ni Afisa yeyote au mtumishi wa Umma aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Chakula" maana yake ni kitu cho chote kinacholiwa au kunywewa na Binadamu isipokuwa madawa hii ni pamoja

na :-

(a) kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula;

(b) kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula;

(c) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula (binzari n.k.)

" Eneo lililo wazi" maana yake ni eneo lililochini ya Halmashauri ya

Wilaya ambalo limekatazwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa;

" Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze;

"Kero" maana yake ni kitu chochoteambacho ni chukizo au kinatumika, au kimewekwa, kimejengwa au ni kichafu kiasi cha kusababisha:-

(a) hatari kwa viumbe au maisha ya wanadamu;

(b) harufu mbaya na ya kuudhi;

(c) magonjwa kwa binadamu, kuhifadhi mbu, inzi, panya na viumbe wenye madhara.

"Mkazi" maana yake ni mtu yeyote au mwananchi ambaye

kwa kawaida anaishi kwenye eneo lililoko chini ya Mamlaka ya Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri.

" Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

" Majani" maana yake ni majani yote marefu, vichaka vyenye urefu wa

sentimenta 15 au zaidi vinavyopatikana sehemu yoyote ndani ya Halmashauri ya Wilaya hii ni pamoja na mazao marefu

" Maji taka" maana yake kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi wa

Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ;

"taka" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004

"Vyanzo vya maji" maana yake ni maziwa, visima vya aina zoteChemichemi na mito

Wajibu

4. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mwenye nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba:-

(a) mazingira yanayozunguka eneo la nyumba yake au

nyumba anayoishi yanakuwa safi wakati wote.

(b)takataka au uchafu wote zinakusanywa na kufukiwa au kuondolewa kwa njia itakayoelekezwa na Halmashauri;

(c) anachimba shimo la kutupia takataka litakalokuwa na upana

usiopungua futi 2 kwa futi 2;

(d) anajenga choo imara chenye upana wa futi 4 kwa 4 kilichojengwa kwa matofali na kuezekwa kwa bati au nyasi na kinachotumika muda wote

(e)anaifanyia nyumba yake matengenezo mara moja inapokuwa imeharibika

(f) eneo lake analofanyia biashara liko katika hali ya usafi na kwa yale maduka ya chakula na dawa yatatakiwa kuwa yamesajiliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA);

(g) eneo linalozunguka halina mazalia ya mbu.

(h)majani yanayozunguka nyumba yake yanakatwa na kufanya usafi katika eneo lake mara kwa mara.

(i) Nyumba yake ni bora na inapaswa iwe na madirisha ya kutosha yenye eneo lisilopungua sehemu kumi ya eneola sakafu ya kila chumba.

Mamlaka ya Afisa Mwidhini-wa

5. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote ndani ya Halmashauri ili kukagua kama kuna kero yoyote na kumtaka mtu anayehusika na kero hiyo kuiondoa katika muda watakaopewa na Afisa Mwidhiniwa.

Wajibu wa watoa huduma

6. Wajibu wa watoa huduma utakuwa kama ifuatavyo;-

(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mhudumu wa hoteli, migahawa baanyumba za kulala wageni, bucha, waoka mikate, watu wanaoshughulikia na kuuza vyakula na vinywaji kwa ajili ya matumizi ya binadamu kuhakikisha kwamba wanapima afya zao mara moja kila baada ya miezi sita.

(2) Kila mmiliki wa hotel,mgahawa,bucha ,bekari na nyumba za kulala wagenu atalazimika kuwa na kibali cha Halmashaurikinachomruhusu kuendesha biashara hiyo atakacholipia ada ya shilingi 5,000/=.

Marufuku

7 1. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuacha wazi shimo la maji machafu au kumwaga maji, au taka, kutapisha au kuruhusu kumwaga taka au kuruhusu kufurika choo, karo, septic tank,au kuruhusu kuziba bomba la maji taka toka ndani ya nyumba na kuyatiririsha kwenye barabara, njia, kichaka, sehemu nyingine

isiyoruhusiwa.

2. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kufungulia muziki kwa kupiga

Sauti ya juu ambayo itasababisha makelele na kuwa kero kwa wakazi Wengine.

3. Itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yote kutengeneza au kuuza Chakula mtaani, uchochoroni, magengeni au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za Afya na awe amepata kibali kutoka katika Halmashauri.

8. Halmashauri itatoa huduma ya kupuliza dawa ya kuua wadudu katika nyumba za biashara,kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi

9. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu ye yote:-

(a) kujenga choo umbali wa chini mita 60 ya kutoka kisimani, ziwani mtoni au chanzo kingine chochote cha maji.

(b) kutiririsha kinyesi au kusababisha kinyesi, mkojo, maji machafu kutiririsha kutoka kwenye choo

chake au bafu lake au karo la kuoshea vyombo au kufulia nguo au kutoka kwenye bomba lo lote linalochukua maji machafu, na kuelekeza kwenye barabara au mitaa au kwenye mifereji ya maji ya mvua au mfereji wowoteulio wazi;

(c) Kutupa takataka au kusababisha mrundikano wa takataka mahali popote pasipo ruhusiwa na Halmashauri.

(d) Kufanya biashara ya chakula au vinywaji bila kibali cha Halmashauri au kufanya biashara hiyo katika eneo lisiloruhusiwa .

Adhabu

10 Mtu yeyote atakayevunja au kushindwa kutimiza masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni moja (Tsh.1000,000/=)au isiyopungua shilingi laki mbili (200,000) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili jela au adhabu mbili yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa kwa ,kiasi kisichopungua shilingi laki mbili (Tsh.200,000/=) na kisichozidi shillingi laki tano (500,000/=) mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo atakiri kosa kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi .

JEDWALI LA KWANZA
HUDUMA YA KUPULIZA DAWA YA KUUA WADUDU

(Chini ya kifunhu cha 8 Sheria Ndogo hizi)

Nyumba za biashara	Kiasi kuanzia shilingi 10,000
Nyumba za kuishi	Kiasi kuanzia shilingi 30,000 kila baada ya miezi 6
Maofisi na majengo mengine	Shilingi 20000 kadri ya mahitaji

JEDWALI LA PILI

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA
(Chini ya kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hizi)

Mimi……wa S.L.P…… ninaefanya biashara ya …… katika eneo la …… lililopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze Nakiri kuwa leo tarehe ……Nilikiuka kifungu cha ……cha Sheria Ndogo za (Usafi wa Mzingira) za Halmashauri ya Chalinze za Mwaka, 2018. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini ……

Jina……

Tarehe …….

Mbele yangu …….

Saini ……

Wadhifa ……

Tarehe ……..

Tangazo la Serikali Na. 741 (Linaendelea.)

Nembo ya Halmashauri ya wilaya ya chalinze imebandikwa kwenye SheriaNdogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe ..... mbele ya:-

EDES PHILIP LUKOA
Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze

L.S

SAIDI OMARI ZIKATIMU
Mwenyekiti Halmashauri ya Chalinze

NAKUBALI,

Dodoma,
4 Octoba, 2018

NAKUBALISELEMANI S.JAFO (MB.)
Waziri Wa Nchi- Or - Tamisemi